JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

***Unapojibu tafadhali taja:***

**Kumb. Na.** BAG/LD/64142/4

Tarehe: 19 Novemba, 2024

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha Uwekezaji (TIC),
S.L.P 938,
**DAR ES SALAAM.**

**Yah: KUOMBA UTHIBITISHO WA UMILIKI WA KIWANJA NA. 87 KITALU 'Q' ENEO LA KIMELE HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO**

Tafadhali husika na kichwa habari hapo juu.

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo inakiri kopokea barua yako yenye Kumb Na. CA.148/234/01H/168 ya tarehe 11 Novemba, 2024 ya kuhusu mada tajwa.

3. Barua hiyo, imeeleza kuwa, mmepokea maombi kutoka Kampuni ya **Chai Leo Limited** ya kusajili mradi wa ujenzi wa Godauni (warehousing) na kupata cheti cha vivutio vya uwekezaji (Certificate of Incentivies). Hivyo, mnaomba Ofisi iwathibitishie umiliki pamoja na matumizi ya ardhi ya kiwanja tajwa.

4. Kulingana na kumbukumbu za Ofisi, kiwanja tajwa hakijamilikishwa isipokuwa Ofisi imepokea barua ya maombi ya kumilikishwa kiwanja tajwa kutoka kampuni ya **Chai Leo Limited**, wakiomba kumilikishwa kupitia utaratibu wa uwekezaji wa kigeni ili waweze kupata haki isiyo ya asili.

5. Aidha, kupitia maombi yao, pamoja na nyaraka nyingine, wameambatisha nyaraka za uthibitisho wa umiliki wa eneo ikiwapo nakala ya mkataba wa manunuzi kutoka kwa Fratern Roman Namfua, nakala ya Muhtasari wa kikao cha Baraza la Kitongoji kilichokaa tarehe 30/09/2024 na nakala ya hati ya kuhakiki mipaka ya ardhi.



CamScanner

6. Matumizi ya kiwanja yanaendana na mradi wa ujenzi wa Godauni (Ware housing) unaokusudiwa kuwekezwa kama ulivyoeleza.

7. Kwa kuzingatia maelezo hapo juu, Ofisi haina pingamizi kwa Ofisi yako kusajili mradi wa Godauni kwa Kampuni ya **Chai Leo Limited** na endapo usajili utakapokamilika tunaomba tufahamishwe ili maombi yao ya kumilikishwa yaweze kufanyiwa kazi.

8. Ahsante.

Shauri Selenda
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**BAGAMOYO**

MKURUGENZI MTENDAJI (W,
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO

**Nakala:-**

Mkurugenzi,
Chai Leo Limited,
S.L.P 35,
**BAGAMOYO.**

FM/DM/ARDHI



CamScanner